



AZIMIO NA. 08/2017

AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA UANZISHWAJI WA KAMISHENI YA PAMOJA YA BONDE LA MTO SONGWE KATI YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA SERIKALI YA JAMHURI YA MALAWI (*CONVENTION ON THE ESTABLISHMENT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA AND THE GOVERNMENT OF THE REPUBLIC OF MALAWI*)

KWA KUWA, Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC);

NA KWA KUWA, Tanzania ni moja ya Nchi zilizoridhia Mkataba wa SADC na Itifaki ya Maji ya Nchi za SADC inayoelekeza uanzishwaji wa vyombo vya ushirikiano katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji;

NA KWA KUWA, Tanzania na Malawi zilishiriki katika majadiliano ya pamoja yaliyofanyika mwaka 1976 kuhusu namna ya kutatua changamoto zinazosababishwa na Mto Songwe kwa madhumuni ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu;

NA KWA KUWA, tarehe 20 Februari, 2004 Tanzania na Malawi zilisaini Hati ya Makubaliano (MOU) ambayo pamoja na mambo mengine ilitoa mamlaka kwa pande zote mbili kuanzisha Kamisheni mbalimbali za pamoja, ikijumuisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe;

NA KWA KUWA, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika majadiliano yaliyoweza kusainiwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe na hatimaye kusaini Mkataba huo katika Mji wa Lilongwe Nchini Malawi tarehe 18 Mei, 2017;

NA KWA KUWA, Bonde la Mto Songwe ndilo linalofanya mpaka kati ya nchi ya Tanzania na Malawi na ambapo Wilaya za Kyela, Ileje, Mbozi, Mbeya Vijijini na Momba nchini Tanzania zimo katika Bonde hilo;

NA KWA KUWA, Mto Songwe umekuwa ukifurika mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa miundombinu, mali na mashamba na hivyo kuleta madhara, hasara na usumbufu mkubwa kwa wakazi wa Bonde hilo;

NA KWA KUWA, mafuriko ya Mto Songwe yamekuwa yakisababisha kuhama hama kwa mkondo wa Mto na hivyo kusababisha wasiwasi wa kiusalama juu ya uwezekano wa kutokea mgogoro wa mipaka baina ya nchi hizi mbili;

NA KWA KUWA, Tanzania na Malawi zinatekeleza Mradi wa Kudhibiti Mkondo wa Mto Songwe (*The Stabilization of the Course of Songwe River Project*) ambao unapendekeza kujengwa kwa mabwawa makubwa matatu ambayo ni Songwe Chini, Songwe Kati na Songwe Juu kwa madhumuni ya kudhibiti mafuriko;

NA KWA KUWA, Ibara ya 2.12 ya Sera ya Taifa ya Maji na Kifungu cha 98 cha Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura ya 331 kwa pamoja zinaipa mamlaka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushirikiana na nchi nyingine katika umiliki, utunzaji na utumiaji wa pamoja wa rasilimali za maji kwa manufaa ya nchi;

NA KWA KUWA, Mkataba huu unalenga kuimarisha usimamizi, uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali ya maji ya Mto Songwe;

NA KWA KUWA, Ibara ya 15 ya Mkataba huu inaeleza kuwa Mkataba huu, pamoja na masharti mengine, utanza kutumika kwa kuzingatia matakwa ya kisheria ya kila nchi, ambapo kwa nchi yetu ili Mkataba wa Kimataifa uanze kutumika, pamoja na mambo mengine ni budi uridhiwe na Bunge;

NA KWA KUWA, Tanzania kuweka saini na kuridhia Mkataba huu pamoja na kuutekeleza itanufaika kisiasa, kiuchumi na kijamii ikijumuisha:-

- (a) Kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kudhibiti mafuriko ambayo yamekuwa yakiharibu kingo za mto na kusababisha mto kuhama na kuathiri mipaka ya nchi hizi mbili;
- (b) Bwawa la Songwe Chini ambalo litajengwa baada ya kusainiwa Mkataba huu litatumika kuzalisha umeme wa Megawati 180.2, kutoa huduma ya maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, hifadhi ya mazingira na utalii na hivyo kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa eneo la Bonge la Mto Songwe; na
- (c) Kuhifadhi mazingira, kurudhisha uoto wa asili, kuzuia mmonyoko wa udongo na kuhifadhi rasilimali za maji kwa matumizi endelevu.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu kwa Tanzania na umuhimu wa kuridhia Mkataba huu, Bunge hili katika Mkutano wa Nane na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*Convention on the Establishment of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Malawi*).

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 7 Septemba, 2017.

Dkt. Thomas D. Kasilillah
KATIBU WA BUNGE